# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

# MRADI WA UBORESHAJI USALAMA WA MILKI ZA ARDHI




## TAARIFA YA MKUTANO WA KITAIFA WA WADAU ULIOJADILI UTEKELEZAJI WA MRADI WA UBORESHAJI USALAMA WA MILKI ZA ARDHI (LTIP) – KATIKA UKUMBI WA JIJI LA DODOMA MTUMBA TAREHE 17/01/2023

## 1.0 UTANGULIZI:

Serikali ilisaini Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi na Benki ya Dunia tarehe 21 Januari, 2021 ambapo utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2023.

Katikia kutekeleza mradi huu wadau mbalimbali watahusishwa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Mtaa/Kijiji. Wadau hawa watahusishwa kupitia vikao mbalimbali vitakavyafanyika kama ilivyoainishwa katika *Stakeholder Engagement Plan* (SEP). Lengo la mikutano hii ni kuwawezesha wadau kupata taarifa ya utekelezaji wa mradi, kutoa maoni na kutoa dira ya utekelezaji wa mradi. Mkutano wa wadau ngazi ya Taifa ni Mkutano ambao unahusisha wadau katika ngazi ya Taifa. Wizara imeandaa mkutano wa kwanza wa ngazi ya Taifa ili kutoa taarifa kuhusu malengo na matokeo ya mradi yanayotarajiwa; kujadili na kushauri utaratibu bora wa ushirikishwaji wa jamii wakati wa uhamasishaji na utekelezaji wa mradi; na kukubaliana namna bora ya kutoa mrejesho kwa mamlaka husika jinsi mradi unavyotekelezwa. Aidha, kupitia mkutano huu wadau walipata fursa ya kuwasilisha uzoefu wao kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya upatikanaji wa haki za ardhi na mazingira katika maeneo yao.

## 2.0 YALIYOFANYIKA KABLA YA MKUTANO

Maandalizi yalifanyika kwa kuainisha wadau muhimu ambao walialikwa katika Mkutano kutoka Wizara, Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wabunge, Bodi za Wataalamu, Makampuni ya Upangaji na Upimaji, Vyuo Vikuu, Taasisi binafsi, watoa huduma za jamii, Jukwaa la Wahariri, waandishi wa vyombo vya habari Viongozi wa Dini na Taasisi za fedha. Aidha Sekretarieti iliandaa bajeti ya kugharamia Mkutano, kutafuta ukumbi, kuandaa ratiba, machapisho, barua za mialiko na kuzisambaza kwa wadau.

## 3.0 MKUTANO WA WADAU

Ratiba ya siku ya Mkutano ilipangwa kuanza saa 1:30 asubuhi katika ukumbi wa Jiji La Dodoma Mtumba ambapo kipindi cha Aridhio kinachorushwa na *Television* ya TBC kilirusha mahojiano waliyofanywa na Mratibu wa Mradi kuhusu Usalama wa Milki za Ardhi nchini. Mahojiano haya yalirushwa mubashara kutokea Ukumbi wa Mikutano wa Jiji la Dodoma.

Aidha, kikao kilianza rasmi wakati Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alipowasili ukumbini na kukaribishwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mratibu wa mradi alitoa utambulisho kwa mgeni rasmi wa wadau waliohudhuria, kisha mshereheshaji alimkaribisha Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili atoe taarifa ya mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi nchini. Aidha, Katibu Mkuu alifafanua lengo la mradi, vipengele vya mradi, matarajio na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi na kisha kumkaribisha mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhutubia wadau wa Mkutano.

Katika Hotuba hiyo, Mh, Naibu Waziri alieleza kuwa mradi huu unalenga kuboresha usalama wa milki za ardhi kwa; kupanga, kupima na kusajili milki za ardhi zipatazo milioni 2.5 zinazojumuisha hati milki 1,000,000 na Leseni za makazi 1,000,000 katika maeneo ya mijini na Hati za Hakimilki za kimila 500,000 vijijini. Aliendelea kufafanua kuwa, kama ilivyoelezwa katika taarifa ya Katibu Mkuu, Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Kimerekani Milioni mia moja hamsini ($150,000,000) sawa na Shillingi za Kitanzania Bilioni 345 na umepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano (5) kuanzia Mwezi Julai, 2022 hadi mwezi Juni, 2027.

Aidha Mhe. Mgeni Rasmi, aliwaomba Wakuu wa Mikoa kusaidia usimamizi bora wa kazi za Mradi zitakazokuwa zinatekelezwa katika Mikoa yao na pia alisisitiza kuwa watakaopata fursa ya kushiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa mradi huu kwa kufanya ama kuishauri serikali*, “Nawaomba mfanye kazi kwa uaminifu na uandilifu wa hali ya juu na kwa kuzingatia uzalendo (Taifa kwanza)”.* Pamoja na hayo, kila mmoja wetu kwa nafasi yake kutimiza wajibu wake kikamilifu ili kuweza kuleta matokeo chanya katika sekta ya ardhi,

Alimalizia kwa kuishukuru Benki ya Dunia kwa ushiriki wao mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Nawaomba wawakilishi wa Benki ya Dunia mlioshiriki mkutano huu mtufikishie salamu

na shukrani zetu kwa uongozi wenu, mashirikiano haya ni alama nyingine inayothibitisha kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo kazini kuiweka nchi katika nafasi yake.

## 4.0 MAWASILISHO YA MADA MBALIMBALI:

Mshereheshaji alitoa fursa kwa wawasilisha mada kuwasilisha mada zao.

**Mada ya kwanza:** *Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi nchini (LTIP)*

Mratibu wa Mradi (PC), alieleza kwa upana mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi Tanzania na utekelezaji wake katika nyanja kuu tatu;

**a) Chimbuko la mradi, malengo mahususi, bajeti na muda wa utekelezaji**

Mratibu alieleza kwamba lengo mahususi ni kuboresha ufanisi katika utawala wa ardhi na kuongeza usalama wa milki katika maeneo ya mradi kwa; kupanga, kupima na kusajili milki za ardhi zipatazo milioni 2.5 zinazojumuisha hati milki 1,000,000 na Leseni za makazi 1,000,000 katika maeneo ya mijini na Hati za Hakimilki za kimila 500,000 vijijini. Hili linaenda sambamba na

- Kuongeza idadi ya miamala itokanayo na nyaraka za umiliki
- Kupunguza muda unaotumika kupata nyaraka za umiliki
- Kuongeza uelewa wa usalama wa ardhi kwa kuzingatia jinsia
- Kuongeza idadi ya watanzania wanaomiliki nyaraka za umiliki
- Kuongeza ufanisi utakaofanya wamiliki kuridhika na mchakato wa uandaaji wa nyaraka za umiliki

**b) Vipengele vya mradi;**

- Kuongeza usalama wa milki za ardhi
- Kujenga mifumo ya usimamizi wa taarifa za ardhi
- Uboreshaji wa miundombinu ya usimamizi wa ardhi
- Ufuatiliaji na tathmini ya mradi
- Masuala ya athari za kimazingira na jamii kwa ujumla katika utekelezaji mradi.

**Mada ya Pili:** *Ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa mradi*

Afisa Mawasiliano wa Mradi aliwasilisha mada kuhusu Ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa mradi na alianza kwa kueleza kuwa Mkutano wa Taifa wa Wadau (NSEP) ni moja kati ya mifumo ya usimamizi wa mradi na mkutano huo ni mojawapo ya vikao muhimu vya mradi vinavyolenga kujadili namna rahisi ya utekelezaji wa mradi. Hiki ni kikao cha kwanza cha aina hii na vitakuwa vikifanyika mara mbili kwa mwaka katika ngazi ya Taifa.

Aliendelea kwa kueleza kuwa malengo makuu ya kikao hichi kuwa:

- Kutoa na kuboresha miongozo ya ushiriki wa wadau;
- Kutengeneza/kuboresha mbinu za mawasiliano baina ya wadau na watekelezaji wa mradi ikiwemo namna sahihi ya kusambaza taarifa;
- Kujadili namna sahihi ya kuwasilisha hoja au malalamiko yanayohusiana na mradi;
- Kutafakari maazimio yatokanayo na vikao ili kuboresha ufanisi wa utendaji wa mradi; na
- Vikao hivi vitakuwa vikifanyika kwa ngazi kuu tatu nazo ni, ngazi ya Kitaifa, ngazi ya Wilaya na katika ngazi ya Kata.

Alimalizia kwa kubainisha wadau muhimu wa Mkutano nakueleza namna za uwasilishaji maoni kwa Kupitia Mikutano ya wadau, Sanduku la maoni katika Halmashauri, Barua, Barua Pepe, Tovuti ya Mradi n.k. Aidha mradi una jukumu la Timu ya Mradi kukusanya na kufanyia kazi maoni/maswali/malalamiko yatakayojitokeza. Mwisho akawataka wadau waanze kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kulingana na majukumu ya mkutano wa wadau yaliyofafanuliwa hapo juu.

## 5.0 MAJADILIANO NA MAAZIMIO:

Wajumbe walimteua Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Arusha ndugu: John Mongella ambaye pia ni mwenyekiti wa umoja wa wakuu wa mikoa nchini, kuwa mwenyekiti wa majadiliano ambapo alitoa fursa kwa wajumbe wote walioshiriki mkutano kutoa michango yao kama itikio la mawasilisho hayo. Wajumbe walichangia kama ifuatavyo:

1. **Vikao vya Wadau**

Wadau wengi walishauri na kuomba kushusha muundo wa vikao hivi vya wadau hadi ngazi ya vijiji na mitaa na visiishie katika ngazi ya Kata**.**

2. **Kutoa elimu ya Manunuzi kwa CSOs**

Wajumbe waliomba elimu ya manunuzi itolewe kwa CSOs kuhusu mfumo wa manunuzi ili kurahisisha utaratibu wa zabuni pamoja na kuangalia upya utaratibu wa kurahisha manunuzi kupitia sheria zilizopo ili kufanya mradi kutekelezeka kwa muda muafaka.

3. **Mabenki kutokua na Imani na Hakimiliki za Kimila (CCRO) kutumika kama rehani katika kupata mikopo**

Kuna suala la mabenki kutoamini au kutotumia hakimiliki za kimila katika utoaji wa mikopo kunadhoofisha umuhimu wa hati hizo. Aliuliza kama elimu ya kutosha imetolewa kwa mabenki kuhusu umuhimu na matumizi ya Hakimilki za Kimila. Hati hizi kama zitakubalika na mabenki katika utoaji mikopo zitaweza kumkomboa mkulima kupitia mradi huu.

4. **Kujengewa uwezo kwa mabaraza ya Ardhi**

Mabaraza ya Vijiji na Mabaraza ya Kata yajengewe uwezo ili yaweze kutoa mashauri ya migogoro ya ardhi kwa haki na kwa wakati pamoja na kuboresha ofisi hizo.

5. **Mabaraza ya Ardhi**

Changamoto ya upungufu wa wenyeviti wa mabaraza ya ardhi itatuliwe na Wizara. Aidha, Wizara ione namna ya kuwajengea uwezo ili mabaraza yawe na watendaji wenye ueledi na wenye taaluma ya ardhi ili waweze kusaidia katika kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao, kwa njia hii migogoro itapungua.

6. **Taarifa/Muhtasari wa Mkutano**

Wajumbe walishauri kwamba muhtasari wa kikao uandaliwe na utumwe kwa wadau wote ndani ya miezi miwili baada ya kikao ili kuweka muendelezo kabla hawajasahau.

**7. Mfumo wa utoaji hakimilki za kimila**

Wajumbe walishauri kuwe na mfumo mmoja unaofanana wa utoaji hakimilki za kimila (consistency) kwa kuwa kila taasisi ina stahili yake jambo ambalo haliko sawa.

**8. Mipango ya matumizi ya ardhi**

Mipango ya matumizi ya ardhi inayoandaliwa kuhakikisha matumizi ya ardhi yote muhimu yanazingatiwa na yaendane na shughuli husika za eneo. Hii itasaidia kuruhusu matumizi endelevu ya ardhi sasa na vizazi vijavyo mfano; maeneo ya malisho, maziko, vivutio, vitega uchumi, kilimo, ufugaji, makazi na maeneo ya athari na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu yatengwe na kusimamiwa katika mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha upanuzi holela wa miji ambao unaingilia ardhi nzuri ya kilimo uthibitiwe.

**9. Mkakati wa kuwafikia jamii za wafugaji na wawindaji**

Kuandaliwe mkakati maalumu wa kuwafikia makundi maalum (vulnerable groups) hususan wafugaji katika mradi huu ili nao wanufaike. Hii itawezesha kupunguza migogoro iliyopo kati ya wakulima na wafugaji.

**10. Wizara kupitia sera na sheria**

Wadau wengi walishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya ardhi ili ziendane na wakati na kuwezesha mradi huu kufanyika kwa ubora zaidi.

**11. Mikutano kuhusisha wadau wengine**

Ilishauriwa mikutano hii ya wadau ihusishe pia vyombo vya ulizi na usalama na wawakilishi wa makundi maalum kama wakulima wa kawaida, wafugaji, wavuvi na vijana. Aidha, uwepo wa nafasi ya sekta nyingine utasaidia kufikia malengo, kudhibiti ongezeko la watu na upangaji wa matumizi ya ardhi usiyojali matumizi mengine muhimu. Pia, wadau wa afya washirikishwe kusaidia masuala ya kiafya na kiuchumi.

**12. Changamoto ya kutokuchuliwa kwa hati**

Ilishauriwa kwamba ni vyema kabla ya kufanya uhamasishaji kufahamu kwanini matokeo madogo (response) katika uchukuaji hati? Ili kusaidia mradi uende vizuri. Hii itasaidia kujua ni aina gani ya uhamasishaji inahitajika. Pia ilishauriwa Mradi uzingatie haki za sekta nyingine zinazohusika na masuala ya ardhi.

***13.* Ujenzi kufuata *Master Plans***

Ilishauriwa, Wizara iunganishe (harmonize) sheria zake ili kuziboresha ziendane na mahitaji ya sasa. Aidha usimamizi wa dhati unahitajika ili kudhibiti ujenzi wa hovyo ambapo majengo hayaendani na hali halisi na hayafuati master *plans*. Kufanya mapitio (review) ya *master plans* kwa maeneo yaliyoainishwa ili kuwezesha uendelezaji unaondana na *master plans*.

**14. Utunzaji wa Mazingira**

Aidha alieleza kwamba jamii za wafugaji na wawindaji zimekua na changamoto kubwa ya kuhamahama na wengine wamekua chanzo cha kuharibu mazingira kwa kukata miti hovyo. Hivyo mradi uhakikishe makundi haya yanaangaliwa kwa kutengewa maeneo ya matumizi yao husika. Aidha, wapewe elimu kuhusu utunzaji wa mazingira. Pia, mradi uwe na kipengele cha kutoa elimu ya upandaji miti katika maeneo yanayotekeleza mradi ili kuboresha mazingira kwa mfano kuwasisitizia wananchi kupanda miti (angalau mitatu 3) na uhifadhi wa misitu.

**15. Ushirikishwaji wa Waandishi wa Habari**

Ilishauriwa kuwashirikisha waandishi wa habari katika utekelezaji wa mradi.

**16. Kuongeza ajira**

Ilishauriwa kwamba, mradi uhakikishe unatoa ajira kwa vijana waliomaliza vyuo nchini wenye fani za masuala ya ardhi.

**17. Utatuzi wa changamoto katika utekelezaji wa mradi**

Wadau walishauri changamoto zitakazoonekana katika utekelezaji wa mradi zitatuliwe ndani ya nchi kwa kutumia Sheria za Tanzania kwa haraka ili kutokwamisha utekelezaji mradi.

**18. Gharama za umilikishaji**

Wadau walieleza kwamba gharama za umilikishaji na kodi mbalimbali za ardhi zifanyiwe mapitio pamoja na kutoa elimu ya kutosha ili wananchi wapate muamko wa umilikishwaji wa ardhi hususani kuchukua hati baada ya upimaji.

**19. Hofu ya Mungu**

Ilishauriwa kwamba pamoja na kusimamia sharia na kanuni, haki zizingatiwe, wahusika wote wawe na hofu ya Mungu na kushauri kauli mbiu itumike: "weledi, uaminifu na hofu ya Mungu ndio msingi wetu"

**20. Vitambulisho vya NIDA katika umilikishaji**

Ilishauriwa kuwepo na ushirikishwaji wa Taasisi za chini zilizopo maeneo ya mradi. Aidha alisisitiza kwamba jitihada zifanyike za upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa (NIDA) ili wananchi wasisumbuliwe au kucheleweshewa milki zao wakati mradi unaendelea.

**21. Kuimarisha mawasiliano**

Ilishauriwa kuwa na mawasiliano rahisi nay a karibu na wananchi na wadau wengine katika utekelezaji wa mradi kwa mfano njia ya meseji kwa wananchi ili wawe na taarifa kwa haraka pamoja na kutumia watu maarufu.

**22. Ushirikishwaji wa CSOs**

Ilishauriwa kwamba, ushirikishwaji wa CSOs uongozeke na kwamba kulingana na ukuwaji wa miji kwa kasi CCRO's zitatumikaje kulinda ardhi? Kwa mfano mradi utalindaje ardhi za vijiji? Kulingana na migogoro ya mara kwa mara ya wafugaji na wakulima, je wameshirikishwa kwa kila hatua ili kupunguza malalamiko?

### 23. Tathmini ya changamoto za kutumia Sekta binafsi

Wadau walitoa hoja kwa Wizara kufanya tathmini ya changamoto za baadhi ya sekta binafsi (kampuni) zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi mingine ya awali ili kuzuia kujirudia kwa makosa na kusababisha ugumu wa utekeleza mradi huu muhimu wenye maslahi makubwa ya Taifa.

### 24. Kuzingatia uhalisia wa maeneo ya kujenga majengo

Ilishauriwa kuzingatia eneo husika la ujenzi na mazingira ya mkao wakati wa kuandaa bajeti za ujenzi wa majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa ili kurahisisha utekelezaji wake kwa ufanisi kwa kuwa mikoa baadhi ya mikoa ipo mbali na vifaa vya ujenzi vinapatikana kwa gharama kubwa.

### 25. Pongezi kwa mkakati wa kuwezesha wanawake

Muwakilishi Kutoka UN-WOMEN alipongeza mkakati wa mradi kuongeza ushiriki wa wanawake katika kumiliki ardhi na kusema wako tayari kushirikiana na mradi ili kuhamasisha wanawake wengi zaidi waweze kumiliki ardhi na kunufaika kupitia mradi huu.

### 26. Hati Milki zinazowekwa rehani katika Mabenki

Ilielezwa kwamba, kumekuwa na miliki pandikizi (double allocation) hivyo, suala hili liangaliwe katika utekelezaji wa mradi huu. Aidha RL’s na CRO’s zimekuwa zikiwekwa rehani katika benki tofauti (benki zaidi ya moja) na wananchi, changamoto hiyo iangaliwe.

### 27. Kutoa kipaumbele kwa wanawake

Ilishauriwa kutoa kipaumbele kwa makundi maalumu kama vile wanawake na walemavu. Aidha viongozi wa dini watumike katika kutoa elimu ya mradi ambapo itasaidia kujenga hofu ya Mungu.

### 28. Kuzingatia suala la elimu kwa umma na makubaliano ya wawekezaji

Ilishauriwa elimu itolewe sana ili kurahisisha utekelezaji mradi huu hususani kufanya wananchi waone umuhimu wa kupata hatimiliki na kuzichukua. Pamoja na hayo alishauri

katika maeneo yenye uwekezaji mradi uzingatie makubaliano ya wawekezaji na nchi ili kufanya usalama wa milki uwe kwa kila mmoja hata waliowekeza kwa makubaliano mbalimbali.

**29. Umuhimu wa kikao cha wadau cha Taifa**

Muwakilishi kutoka Benki ya Dunia alieleza kwamba wadau watambue kwamba mradi huu ni wa Watanzania na sio wa Benki ya Dunia. Hivyo ni jukumu kwa wadau kuhakikisha wananchi wanaondokana na dhana hii. Aidha alieleza kwamba kikao hiki cha Taifa sio kikao pekee cha kuwahusisha wadau bali kutakua na vikao katika kila ngazi ya utekelezaji wa mradi katika kila shughuli ya mradi kulingana na mahitaji. Alieleza kuwa vikao hivi ni sehemu ya utekelezaji wa mradi hivyo ni muhimu sana na kila mdau anatakiwa kuvipa uzito.

**30. Kuwepo kwa ardhi ya akiba**

Mwenyekiti wa majadiliano alitoa ushauri wa kuwepo kwa ardhi ya akiba ya kutosha ili iweze kutumiwa na wawekezaji pindi itakapohitajika.

**31. Mapungufu yaliyopo ya makampuni ya urasimishaji**

Ilishauriwa kuwa, kwa kuwa mradi huu unakwenda kutumia makampuni binafsi ya urasimishaji ambayo yamekuwa na baadhi ya changamoto za kiutendaji, Wizara ijitahidi changamoto hizo zisijirudie katika mradi huu.

**32. Wizara inangalie suala la maendeleo endelevu ya mradi**

Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri 41 wakati nchi ina halmshauri 184, kuna mpango gani wa kufikia maeneo mengine nchini?

## 6.0 UFAFANUZI WA BAADHI YA HOJA

### Ufafanunuzi kuhusu Mabaraza ya Ardhi

Msajili wa Mabaraza ya Ardhi alitoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja kwa kueleza kwamba mabaraza ya Kata yanasimamiwa na Mkurugenzi wa Hamashauri. Wizara itatoa elimu ya

kuwezesha kwa kupewa miongozo wajue wanachokifanya katika kupunguza au kuondoa migogoro ya ardhi.

**Mratibu wa Mradi (Project Coordinator)** aliwaeleza wadau kwamba maoni yamepokelewa na yatafanyiwa kazi kulingana na majadiliano ya wadhamini (Benki ya dunia). Alieleza kwamba majengo ya kusomea ya chuo cha ardhi Tabora na Morogoro yatajengwa kama ilivyoainishwa kwenye nyaraka za mradi.

## 7.0 MAAZIMIO NA KUFUNGA MKUTANO

Wajumbe waliazimia kuwe na utaratibu wa utoaji wa maoni wakati wowote inapohitajika, isisubiriwe siku ya kikao tu; walishauri njia ya kutoa maoni iainishwe ili waweze kuendelea kutoa maoni yao.

## 8.0 KUFUNGA MKUTANO

Pamoja na majadiliano tajwa hapo juu Mhe. Katibu Mkuu alihitimisha ifuatavyo: -

- Maoni yamechukuliwa utaratibu wa mrejesho utatolewa;
- Katika mradi, Wizara inakiri mapungufu yapo katika makampuni ya urasimishaji hivyo, muongozo unaandaliwa ili kusahihisha changamoto na kuchukua hatua kwa wakati;
- Umuhimu wa kuboresha usalama wa milki za ardhi umeonekana, hivyo Wizara itaongea na Benki ya Dunia (WB) kuandaa mkakati na programu kwa nchi nzima;

Katibu Mkuu alihitimisha kikao kwa kuwashukuru wadau wote waliohudhuria na kutoa michango yao ambayo itaboresha utekelezaji wa mradi na alifunga kikao saa 10:30 jioni.

## SEHEMU YA PILI YA MKUTANO KATIKA VIWANJA VYA BUNGE TAREHE 21/01/2023

Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii na wale wanaotoka katika majimbo yanayotekeleza mradi katika awamu ya kwanza ni miongoni mwa wadau muhimu katika Mikutano ya Taifa. Kutokana na ratiba ya Mkutano wa wadau wa Kitaifa kuingiliana na ratiba ya vikao vya kamati za Bunge ilikubaliwa kuwe na kikao maalumu cha wabunge ili waweze kupata taarifa ya mradi na kujadili utekelezaji wa mradi huu.

Katika kikao hicho ambacho kilihudhuriwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Wakuu wa Idara na baadhi ya wajumbe wa timu ya utekelezaji wa mradi. Mratibu wa mradi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi.

Wabunge walipata nafasi ya kuchangia mambo mbalimbali yatayoboresha utekelezaji wa mradi na mengine ya kupata ufafanuzi kutokana na wasilisho. Mambo yaliyochangiwa na wabunge ni kama ifuatavyo;

- Msisitizo wa kuangalia uwezekana wa kuongeza hati za kimila kwa kuongeza idadi ya vijiji na Wilaya ili kupunguza kiu na matatizo ya msingi ya wananchi walio wengi;
- Kuhamasisha wanawake kushiriki katika shughuli za mradi;
- Kutoa elimu juu ya umuhimu wa wanawake kumiliki ardhi;
- Kuboresha Mabaraza ya Ardhi ili yaweze kushughulikia migogoro kwa wakati;
- Kuongeza mikoa katika maeneo ya utekelezaji wa mradi;
- Kuzingatia masuala ya jamii na mazingira (safeguards);
- Kuona ni jinsi gani familia zilizopo katika ndoa ya wake wengi, wanawake wanaweza kumiliki ardhi kwa pamoja;
- Gharama za umilikishaji wa ardhi ziangaliwe; na
- Kuhusisha kundi la wafugaji/wawindaji katika maeneo ya mradi ili kupunguza migogoro.

……………………….

**Tarehe**

…………………………………

Dr. Allan Kijazi

**Katibu Mkuu**
**Mwenyekiti**

………………………………

Joseph I. Shewiyo

**Mratibu wa Mradi**
**Katibu**

## PICHA ZA MKUTANO WA WADAU












